**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI HIYO MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
**DODOMA**

APRILI, 2018

**YALIYOMO**


**1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1**
**2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ................................................... 3**
2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyolengwa kukaguliwa ................................. 3
2.1.1 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF) ........................................................................................ 4
2.1.2 Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) .................................... 6
2.1.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).................................................. 8
2.2 Matokeo ya Ukaguzi......................................................................................... 8
2.2.1 Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini "Support to Tanzania Social Action Fund" ........................................................................ 9
2.2.2 Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) .................................................................. 12
2.2.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)................................................ 14
2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 ...................................................................... 15
**3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 .......................................................................... 18**
3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ...................................................................... 18
3.1.1 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ................................................. 18
3.1.2 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ....................... 21
**4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ........................................... 23**
4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 .............. 23
4.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ....................................... 27
**5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ................................................................ 32**
**6.0 HITIMISHO............................................................................................. 36**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA, KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI HIYO MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na 117 (11) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Ili kukidhi masharti ya Kifungu cha 6(4) pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ilipitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya uchambuzi wa bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka

wa fedha 2017/2018. Ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Bunge. Baada ya hatua hiyo, Kamati ilijielekeza katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2017/18 na kulinganisha na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Taarifa hiyo inahusisha jumla ya Mafungu Nane (8) yafuataо:-

i) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;
ii) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
iii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma;
iv) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
v) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;
vii) **Fungu 09:** Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na
viii) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejikita katika maeneo manne yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyolengwa kukaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa **Tsh. 390, 970, 890, 000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu matano kama ifuatavyo:-

**i)** **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – **Tshs. 379,570,890,000/=**;

ii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma – **Tshs. 7,000,000,000/=**;

iii) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – **Tshs. 1,650,000,000/=**;

iv) **Fungu 67**: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - **Tshs. 750,000,000/=**; na

v) **Fungu 4:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa – **Tshs. 2, 000,000,000/=**.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuzingatia sharti la kikanuni linalozitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa kipindi kisichozidi siku Saba (7), Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Miradi iliyotembelewa inahusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC). Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF)

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 378,570,890,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1003 cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mradi huu ambao unatekelezwa katika mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar, uko katika awamu ya tatu ya utekelezaji wake ambayo imejikita kusaidia kaya maskini za Watanzania kujimudu kiuchumi kwa kupunguza umaskini wa

kipato; kuboresha maisha na ustawi wa jamii, na kuhamasisha uwajibikaji na kuzingatia dhana ya utawala bora.

Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, tangu kuanza kwa awamu ya tatu ya TASAF takribani Watanzania **milioni 5** kutoka kaya maskini 1,118,751 wameandikishwa na wananufaika na ruzuku. Aidha, jumla ya **shilingi bilioni 147.6** zilitolewa kama ruzuku kwa kaya maskini zilizoandikishwa kupitia mpango huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa zaidi kuwa mpango huu umetoa ajira za muda kwa kaya za walengwa 288,385 kupitia utekelezaji wa miradi 3,682 yenye thamani ya **shilling bilioni 13.3.** Miradi hiyo inatekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar kwa kuhusisha Vijiji 2,091, Mitaa 331 na Shehia 168.

Aidha, zoezi la uhakiki wa kaya maskini kwa lengo la kuhakikisha wanaonufaika ni wale wenye sifa stahiki, limekuwa likifanyika muda wote na hadi kufikia mwezi Februari, 2018 kaya zipatazo 7,573 zilibainika kukosa sifa, hivyo kuondolewa katika mpango huu.

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu Kamati ilitembelea na kukagua Mitaa ya Nyalikungu na Mnadani na Kijiji cha Shanwa, Wilayani Maswa, mkoani Simiyu.

2.1.2 **Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa jumla ya **shilingi 1,500,000, 000/=** na unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 kiitwacho *"Policy and Planning"* cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mpango huu umeendelea kuandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa raslimali na uendeshaji wa biashara unaotambulika na kukubalika kisheria. Kupitia mpango huu wanyonge wanawezeshwa kurasimisha mali walizonazo (ardhi na biashara) na kuzitumia kujikwamua kiuchumi.

Kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, MKURABITA imewajengea wakulima 589 na viongozi 89 uwezo wa kutumia Haki Miliki za Kimila ili kupata mitaji katika benki na taasisi zingine za fedha katika Halmashauri za Wilaya za Misungwi, Mpwapwa na Serengeti.

Aidha, wafanyabiashara 870 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara katika Wilaya ya Urambo, baada ya MKURABITA kushirikiana na Halmashauri ya wilaya hiyo kuanzisha kituo kimoja cha urasimishaji wa biashara (*one stop formalization centre*). Kupitia kituo hicho, wananchi wananufaika kwa kupata sehemu moja huduma za leseni za biashara, Namba ya Utambulisho

wa Mlipa kodi (TIN), ujasili wa jina la biashara (BRELA), huduma za kibenki na mifuko ya hifadhi ya jamii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Zanzibar jumla ya wafanyabiashara 100 katika Wilaya za Kusini Unguja (50) na Micheweni, Pemba (50) wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara. Kati ya hao wafanyabiashara 10 wamefanikiwa kusajili majina ya biashara na kupata leseni za biashara.

Aidha, MKURABITA kwa kushirikiana na Ofisi za Taifa za Takwimu Tanzania Bara na Zanzibar, imeanza kufanya utafiti kuhusu sekta isiyo rasmi kwa lengo la kubaini ukubwa na thamani ya sekta hiyo kwa sasa. Utafiti wa majaribio umefanyika katika mikoa Sita (6) ya Tanzania Bara (Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Tanga) na mikoa miwili (2) ya Zanzibar (Mjini Magharibi na Kusini Pemba), ili kuona kama methodolojia, sampuli na madodoso yaliyoandaliwa yanaweza kuleta matokeo tarajiwa juu ya ukubwa wa sekta isiyo rasmi kwa sasa. Vilevile, utafiti mkubwa unaendelea kufanyika nchi nzima kuanzia Machi hadi Juni, 2018 na matokeo yake yatatolewa katika ngazi ya mkoa na taifa.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitembelea Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga ili kujiridhisha kuhusu hali ya utekelezaji wa MKURABITA.

### 2.1.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika,** chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala. Aidha, chuo kinajihusisha na utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam na kutoa machapisho mbalimbali ya kitaalam kwenye utumishi wa Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo kupitia Kampasi Sita (6) zilizoko katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara, Singida, Tanga na Tabora.

Ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo hiki na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ilitembelea Kampasi ya Tabora ambayo ilikuwa ikitekeleza ukarabati wa jengo la Shaban Robert.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni muhimu kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya ukaguzi huo. Kwa madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na majedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Ofisi hii. Ufafanuzi wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 **Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini "Support to Tanzania Social Action Fund"**

**Mheshimiwa Spika**, katika Wilaya ya Maswa, Kamati ilitembelea Kijiji cha Shanwa ambacho kina jumla ya Kaya 248 zinazonufaika na utaratibu wa kunusuru kaya maskini. Idadi hiyo ya kaya imepungua kwa asilimia 19 ikilinganishwa na kaya 308 zilizokuwa zinanufaika awali, kabla ya zoezi la uhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa. Kaya hizo zimepokea ruzuku ya jumla ya **shilingi bilioni 8.85** kutokana na awamu 16 za malipo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile TASAF imeshiriki kwa kiasi kikubwa katika kuboresha elimu ya Sekondari kwa kuchangia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Sekondari Nyalikungu kwa kutoa jumla ya **shilingi milioni 29.6.**

Aidha, kupitia utaratibu wa kuwezesha mahudhurio ya shuleni kwa watoto wanaotoka kaya maskini, mfuko huu umewezesha **Wanafunzi 49** kushiriki kikamilifu katika masomo yao ya sekondari. Wanafunzi hao walio katika kidato cha kwanza hadi cha nne wanalipiwa gharama za masomo na mfuko huu, ambazo ni pamoja na sare za shule, madaftari, kalamu, viatu na matumizi mengine.

Kupatikana kwa mahitaji hayo muhimu kumesaidia kuboresha mahudhurio shuleni, na hivyo kupunguza utoro na mdondoko (drop out) kwa wanafunzi hao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishuhudia namna ambavyo baadhi ya wanufaika wa mpango wametumia fedha za ruzuku kujenga na kuboresha makazi yao. Miongoni mwa wanufaika hao ni Bibi Monica Katambi Gwilasa (miaka 60), ambaye ametumia ruzuku kama chachu ya kujenga nyumba ya tofali ya vyumba vitatu na kuezeka kwa bati.

Mnufaika huyo alieleza Kamati jinsi alivyogeuza ruzuku aliyokuwa akiipata kuwa mtaji na kuanzisha biashara ndogo ndogo zilizompatia kipato na hivyo kuweza kujenga nyumba hiyo.

Kamati ilitaka kujua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza. Kutokana na ukaguzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

**a) Mafanikio;**

i) Kupungua kwa kiwango cha umaskini katika kaya kutokana na ongezeko la upatikanaji wa mahitaji ya msingi;

ii) Ongezeko la idadi ya watoto wanaoandikishwa shuleni;

iii) Kupungua kwa tatizo la ajira za watoto wadogo;

iv) Watoto kutoka Kaya maskini zinazonufaika wanapata mahitaji muhimu ya shule na hivyo kuhudhuria shuleni kwa zaidi ya asilimia 80;

v) Walengwa wa mpango wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile, kilimo, ufugaji na biashara na kuongeza kipato ambacho kimewasaidia kuboresha maisha;

vi) Ongezeko la mahudhurio ya kliniki kwa watoto wa chini ya miaka mitano (5) kutoka asilimia 80 hadi 97; na

vii) Walengwa wengi kutumia sehemu ya ruzuku kujiunga katika Bima ya Afya ya Jamii (CHF) na hivyo kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya.

**b) Changamoto;**

i) Mahitaji makubwa ya fedha za usimamizi wa mpango ikilinganishwa na kiasi kinachopokelewa;

ii) Walengwa wengi wa mpango kuhamia maeneo mengine bila kutoa taarifa kwa uongozi;

iii) Malalamiko kutoka kaya maskini ambazo hazijaingizwa kwenye mpango;

iv) Fomu za utimizaji wa masharti ya afya na elimu kutojazwa kwa usahihi; na

v) Baadhi ya wanakamati wa CMC kujitoa kutokana na ujira/posho kidogo wanayoipata.

### 2.2.2 Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

**Mheshimiwa Spika,** katika Halmashauri ya Msalala ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa MKURABITA, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto. **Jedwali Na. 01** linatoa muhtasari wa hali utekelezaji wa mpango huu.

**Jedwali Na. 01: Mashamba yaliyopimwa katika vijiji vya Lunguya na Segese na Lunguya**

| Na. | Kijiji | Mashamba yaliyopimwa | Hati zilizotolewa | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Lunguya | 1047 | 205 | 19.58 |
| 2. | Segese | 1111 | 60 | 5.4 |
| **Jumla** | | **2158** | **274** | **12.69** |

**Chanzo:** Taarifa za MKURABITA kuhusu urasimishaji wa ardhi na biashara.

## a) Mafanikio

i) Kupungua kwa migogoro ya ardhi katika vijiji hivyo;

ii) Kuongezeka kwa usalama wa milki ya ardhi za wakulima waliorasimisha ardhi yao;

iii) Wanawake wamemilikishwa hati miliki za ardhi peke yao au pamoja na wenza wao;

iv) Baadhi ya wananchi wamekuza mitaji ya biashara kutokana na mikopo waliyoipata kwa kutumia Hati Miliki za Kimila kama dhamana; na

v) Mafanikio katika vijiji hivi yamekuwa chachu ya kuendeleza urasimishaji katika vijiji vingine 14 ambapo mashamba 24 yamepimwa na Hakimiliki kuandaliwa;

a) **Changamoto;**

i) Ukosefu wa fedha unakwamisha utekelezaji wa MKURABITA;

ii) Ukosefu wa Afisa Ardhi Mteule wa kusajili Hati Miliki za Kimila, unachelewesha kukamilika kwa hati hizo. Mfano; katika urasimishaji uliofanyika mwaka 2014 Hati Miliki zake zimetolewa mwaka huu, 2018.

iii) Upotevu wa takwimu za ardhi na kukosekana kwa Wataalam kutokana na mgawanyiko wa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, iliyozaa Msalala na Ushetu;

iv) Kasi ndogo ya utayarishaji wa Hati Miliki kutokana na uhaba wa Watumishi wa Ardhi; Mfano, katika maeneo yaliyotembelewa na Kamati, kati ya mashamba 2158 yaliyopimwa ni Hati Miliki 274 tu (sawa na asilimia 12.69) ndiyo zimeandaliwa;

v) Baadhi ya Wananchi kushindwa kugomboa Hati za Miliki za Kimila za maeneo waliyopimiwa;

vi) Wamiliki wa Hati za Hakimiliki za Kimila kukosa ujuzi wa kuandaa maandiko ya miradi ambayo yatawawezesha kupata mikopo kutoka benki na taasisi nyingine za kifedha.

### 2.2.3 **Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Utumishi wa Umma, kilianzishwa mwaka 2000 baada ya kuunganishwa kwa Chuo cha Uhazili Tabora *(Tabora Secretarial College*) ambacho kilianzishwa rasmi mwaka 1973 kwa ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Sweden, na Chuo cha Watumishi wa Serikali (*Civil Service Training Centre*) kilichokuwa Dar es Salaam.

Kwa sasa chuo hiki chenye Kampasi Sita ambazo ziko mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara, Singida, Tanga na Tabora, ni nguzo muhimu ya mafunzo ya kiutumishi kwa Watumishi wa Umma.

Katika ziara yake, kwenye Kampasi ya Tabora Kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Chuo kinamiliki maeneo yake na kipo katika hatua za mwisho za kupata Hatimiliki. Hii ni tofauti na Kampasi nyingine kama vile Mbeya na Tanga ambazo zinatumia majengo ya kupanga;

ii) Chuo kina upungufu wa watumishi wa kudumu, vitendea kazi na vyumba vya madarasa;

iii) Uchakavu wa miundombinu ya maji na umeme unaongeza gharama za uendeshaji;

iv) Upungufu wa vitendea kazi na vyumba vya madarasa; na

v) Mwitikio hafifu kutoka Wizara na Taasisi za Umma katika kutumia huduma za chuo hicho;

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba:-

i) Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini utafanikiwa zaidi iwapo fedha za ndani zitatumika kiasi kikubwa kama ilivyo kwa fedha za Wafadhili. Bado mchango wa Serikali ni mdogo kwani tangu kuanza kwa mpango huu katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imechangia **Shilingi bilioni 4.35** kati ya zaidi ya **shilingi bilioni 63.5** ilizopaswa kuchangia hadi sasa, kiasi ambacho ni sawa na asilimia **6.85**;

ii) Wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini wanaweza kujikwamua kiuchumi iwapo watatumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi midogo midogo ya kiuchumi

kama vile biashara, ufugaji au kilimo. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Jamii katika halmashauri isaidie kuwaelimisha walengwa hao;

iii) Iwapo TASAF itahakiki na kusajili Kaya maskini zilizosahaulika katika Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, itasaidia kupunguza au kuondoa malalamiko miongoni mwa Jamii;

iv) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umechangia kuboresha mahudhurio ya Watoto wa Kaya maskini shuleni na kliniki. Mfano; Wanafunzi 49 katika Shule ya Sekondari Nyalikungu (Wilayani Maswa) wanahudhuria kikamilifu masomo kutokana na mpango wa ruzuku kwa kaya maskini;

v) Hatua ya Vituo na Zahanati binafsi kukataa kuwahudumia wanachama wa Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) kunakatisha tamaa wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini ambao waliamua kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kujiunga na CHF;

vi) Zoezi la kuhakiki na kuondoa watu wasio na sifa katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, litafanikiwa iwapo litashirikisha wanajamii, viongozi wa Serikali za Mitaa na kuzingatia haki;

vii) Bajeti finyu kwa MKURABITA inaanthiri utendaji wa mpango huo na hivyo kukwamisha zoezi la urasimishaji;

viii) Watendaji wa Halmashauri waliojengewa uwezo na MKURABITA, wanaweza kuendeleza zoezi la urasimishaji iwapo watawezeshwa kwa kupatiwa vifaa na raslimali fedha;

ix) Benki na taasisi za fedha zikielimishwa kuhusu hadhi ya Hati za Hakimiliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo, zitatoa mikopo kwa Wananchi wanaomiliki ardhi kwa hati hizo;

x) Halmashauri zikipatiwa wataalam wa ardhi, zitasaidia MKURABITA kuharakisha zoezi la kurasimisha ardhi na kutoa Hati za Hakimiliki kwa wahusika;

xi) Iwapo Mfuko wa Kujitegemea wa Rais utatengewa fedha za kutosha utaweza kufikisha huduma zake katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kunufaisha Wanawake na Vijana wengi zaidi;

xii) Iwapo Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Tabora kitapatiwa watumishi wa kudumu, na vitendea kazi kitaboresha huduma na kupunguza gharama kulipa watumishi wa mkataba na washiriki;

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ulijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa. Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

#### 3.1.1 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa:-

i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji fedha (cash flow plan);

ii) Fedha zinazotolewa kutoka Hazina kwa ajili ya maendeleo ni pungufu kwa asilimia 14 ikilinganishwa na fedha za matumuzi ya kawaida; na

iii) Fedha hazipatikani kwa wakati na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Ofisi hii.

Maelezo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (na mafungu yake) kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2018 (kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2017/18) na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi zaidi umebainisha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake, ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 417, 779, 331, 561/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 50.89** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Kamati ililinganisha hali hiyo ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2017/2018 na mwaka 2016/2017 na kubaini kuwa kiasi hicho cha fedha kimepungua kwa takribani **shilingi 109,336,885,951** (sawa

na asilimia **20.74)** ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/17 ambacho kilikuwa ni **shilingi 527,116,217,512**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebainisha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mafungu yake, ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 206,720, 967,511/=** kutoka Hazina. Kiasi hicho ni sawa na asilimia **52. 87** ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

Kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa **asilimia 16.26** ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya maendeleo ambacho kilikuwa ni **shilingi 246,780,369,584/=**.

Aidha, Kamati imebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla haukuwa mzuri, kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani asilimia **50.37** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Kwa tafsiri rahisi ni kwamba, kiasi kilichopaswa kupatikana kwa kila robo ya mwaka wa fedha hakikuweza kupatikana. Kwa kuzingatia asilimia 25 ya bajeti kwa kila robo, ilitarajiwa kwamba hadi kipindi hicho fedha iliyoidhinishwa ingekuwa imepatikana kwa takribani **asilimia 70**.

Vilevile, katika kipindi hicho jumla **shilingi 298,604,842,833/=** zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi ambacho ni sawa na asilimia **69.39** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Tafsiri ya mwenenendo huo ni kwamba,

kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kilikuwa kikubwa zaidi ikilinganishwa na fedha za maendeleo zilizopatikana katika kipindi kama hicho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka Hazina siyo mzuri ikilinganishwa na miaka iliyopita kwani, kiasi kinachotolewa kimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Aidha, kasumba ya fedha za matumizi ya kawaida kuwa nyingi ikilinganishwa na fedha za maendeleo imeendelea kuwepo.

### 3.1.2 **Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri katika mambo Ishirini na Moja (21) kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imezingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kuzingatia yaliyosalia. Baadhi ya maoni na ushauri vilivyozingatiwa ni kuhusu:-

i) Serikali kutoa mchango wake wa fedha katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo katika

mwaka huu wa fedha Serikali imetoa jumla ya **shilingi milioni 750** kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo;

ii) Baadhi ya Taasisi za kifedha kutokuwa tayari kutoa mikopo kwa dhamana ya Hati za Hakimiliki za Kimila; ambapo MKURABITA imeanza kuelimisha na kuhamasisha benki na taasisi za kifedha kuhusu uhalali wa hati hizo kama dhamana kwa ajili ya mikopo. Aidha, taasisi hizo za fedha zinatumika kuwaelimisha wamiliki wa ardhi wenye hati hizo namna ya kuandaa mpango kazi kuhusu mikopo watakayoichukua. Tayari wakulima 105 kutoka Halmashauri ya Wilaya za Kilosa na Mji wa Njombe wamekopeshwa **shilingi bilioni 3.8** kutoka Benki ya Kilimo kwa dhamana ya hati hizo;.

iii) Kuongeza bajeti ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ambapo katika mwaka ujao wa fedha Serikali imeongeza jumla ya **shilingi bilioni 2.95** kwa chombo hiki.

iv) Serikali iajiri watumishi ili kuziba pengo lililosababishwa na kuondolewa kwa watumishi wasio na sifa baada ya uhakiki wa Watumishi, ambapo Serikali imeanza na inakamilisha utaratibu wa kuajiri watumishi 52,436.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa fedha 2018/2019, kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayojumuisha Mafungu Nane (20; 30; 32; 33; 67; 94; 09 na 04) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 ya Chama Tawala, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla ofisi hii pamoja na mafungu yake imepanga kutekeleza malengo **209** katika mwaka ujao wa fedha na baadhi ya malengo ni pamoja:-

i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake;

ii) Kumshauri Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kikanda, Kimataifa na maeneo mengine;

iii) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) kwa kushirikisha wadau wa sekta ya Umma na sekta binafsi;

iv) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);

v) Kuifanyia mapitio Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya 2007 ili kujumuisha makosa ya uhujumu uchumi na kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa na ufisadi;

vi) Kufuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo kwenye Taasisi za Umma zinazotolewa na Serikali na Wabia wa Maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

vii) Kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na hivyo kujenga jamii inayochukia rushwa;

viii) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa Kaya maskini zipatazo 355,000 katika Vijiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96, ambazo hazikufikiwa katika awamu ya kwanza;

ix) Kuanzisha Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Maendeleo ya Serikali Mtandao, Makao Makuu Dodoma;

x) Kuendelea kupokea na kuhakiki matamko ya viongozi wa Umma kuhusu raslimali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Matamko haya sasa

yanajazwa kwa njia ya mtandao (*online application*) baada ya kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili *(Ethics Management Information System* - *EMIS*).

xi) Kuandaa taarifa nne (4) za gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kima cha chini cha mshahara wenye staha. Taarifa hizi zitawezesha kushauri kuhusu mshahara wa chini unaoendana na gharama halisi za maisha; na

xii) Kuweka na kuhuisha Mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za kiutendaji *(Keyword Filling System)* za Watumishi *(Personanel Records Management System)* katika Taasisi za Umma 58 ili kuboresha utoaji wa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** ili iweze kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 669,094,556,009.** Kati ya fedha hizo **shilingi 473,118,195,009.** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi 195,973,361,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **shilingi 34,247,334,360** sawa na asilimia 7.23 ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 438,870,860,649** sawa asilimia 92.77 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwa kuidhinishwa katika mwaka ujao wa fedha imepungua kwa **shilingi 152,227,791,665** (asilimia 18.53) ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/18 ambayo ilikuwa **shilingi 821, 322, 347, 674.**

Kiasi cha fedha kilichopungua ni kikubwa zaidi kwani ni takribani mara tatu ya kiasi kilichopungua katika mwaka wa fedha unaoisha ambacho kilikuwa ni asilimia **6.89**.

Aidha, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, uchambuzi umebaini kwamba kiasi kinachoombwa kuidhinishwa kimepungua kwa **shilingi 194,997,529,000** (asilimia 49.88) ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 390,970,890,000** kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/18.

Uchambuzi umebaini zaidi kwamba, kiasi kilichopungua ni kikubwa sana kwani ni zaidi ya mara tatu ya kilichobainika kupungua katika mwaka wa fedha unaomalizika ambacho kilikuwa **asilimia 16.13**

## 4.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kufanya ulinganisho na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Uchambuzi wa Kamati ulilenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la Bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji, na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Mambo yaliyobainika ni haya yafuatayo:-

i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ni **shilingi bilioni 669** ni sawa na asilimia 2.06 ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2017/18 ni **shilingi bilioni 32,476;**

ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/19 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 2.45, ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2017/18; lakini bajeti ya jumla ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,

kwa mwaka wa fedha 2018/19 imepungua kwa asilimia 18.59 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa fedha 2017/18;

iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 0.06 katika fedha za maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2018/19, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo ni sawa na asilimia 0.60 ya Bajeti ya Taifa, imepungua kwa asilimia 49.88 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2017/18. Aidha, **Jedwali Na. 02** linafafanua zaidi juu ya ulinganisho baina ya maeneo hayo mawili.


**Jedwali Na. 02:** Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais (UUB) dhidi ya Bajeti ya Taifa, kwa Mwaka 2018/19

| **BAJETI KUU YA TAIFA 2017/2018** | | | **BAJETI YA OFISI YA RAIS – UUB 2017/2018** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mgawanyo** | **Bajeti Kuu (Tsh.Bilioni)** | **Asilimia ya Jumla ya Bajeti kuu** | **Mgawanyo** | **Bajeti ya Wizara** | **Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara** |
| OC | 2895 | 8.92 | OC | 438,870,860,649 | 65.59 |
| Deni la Taifa | 9,705 | 29.88 | - | - | - |


| **BAJETI KUU YA TAIFA 2017/2018** | | | **BAJETI YA OFISI YA RAIS – UUB 2017/2018** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mgawanyo** | **Bajeti Kuu (Tsh.Bilioni)** | **Asilimia ya Jumla ya Bajeti kuu** | **Mgawanyo** | **Bajeti ya Wizara** | **Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara** |
| Mishahara | 7,627 | 23.49 | Mishahara | 34,247,334,360 | 5.12 |
| Maendeleo | 12,248 | 37.71 | Maendeleo | 195,973,361,000 | 29.29 |
| **Jumla** | **32,476** | **100** | **Jumla** | **669,094,556,009** | **100** |

**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa, na Randama ya Ofisi ya Rais – UUB

Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yanaweza kuoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01** na **Na. 02** kama ifuatavyo:-




**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19




**Chati Na. 02: Bajeti ya OR - UUB kwa ajili ya Mis Matumizi Mengineyo na Maendeleo kwa Mw 2018/19**

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

i) Zoezi la kutambua na kuandikisha kaya maskini katika maeneo ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mradi wa ruzuku kwa kaya maskini, lifanyike mapema ili kaya maskini katika maeneo hayo kunufaika na mpango wa ruzuku. Takwimu zinaonesha yapo maeneo ya Vijiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mpango;

ii) Serikali iwezeshe wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini walioamua kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), kutumia kadi hizo kupata huduma ya matibabu nje ya maeneo waliyosajiliwa. Aidha, kadi hizo zitambuliwe kwenye Hospitali/Vituo vya Afya na Zahanati binafsi kama ilivyo kwa aina nyingine za bima za afya;

iii) Serikali ianze maandalizi ya kuwezesha mpango wa ruzuku kwa kaya maskini kuwa endelevu (*Business Continuity Plan – BCP*) ili uendelee hata baada ya Wafadhali kujiondoa katika kuchangia. Iwapo hili halitafanyiwa kazi mapema, ipo hatari ya kuzuka taharuki miongoni mwa wanufaika iwapo mpango utasita ghafla;

iv) Serikali ipunguze urasimu katika kuthibitisha watumishi wa nafasi za uteuzi. Kamati imebaini kwamba, baadhi ya watumishi katika ofisi za umma wamekuwa wakikaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miaka miwili, kwa madai ya kusubiri upekuzi "vetting". Hali hiyo inawavunja moyo watumishi nao na kuathiri utendaji wao kwani hushindwa kufanya maamuzi ya msingi;

v) Serikali iongeze mshahara kwa Watumishi wa Umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka kila kukicha. Sote ni mashahidi kwamba, Serikali haijaongeza mshahara wa Watumishi wa umma kwa mwaka wa tatu sasa;

vi) Halmashauri zitumie Maafisa Maendeleo ya Jamii kuelimisha wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini namna wanavyoweza kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kujikwamua kiuchumi. Baadhi ya maeneo walengwa wamefanikiwa kuanzisha kilimo na ufugaji kwa kutumia sehemu ya ruzuku hiyo;

vii) Kwa kuwa wazee wengi katika vituo vya kutunzia Wazee hawajimudu kiuchumi na hivyo kuwa na vigezo vya kunufaika na mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, Kamati inashauri Serikali iangalie namna ya kuwawezesha Wazee katika vituo hivyo kunufaika na mpango huo;

viii) Zoezi la kuhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, litekelezwe kwa uangalifu ili kuepuka uonevu na malalamiko kutoka kwa waathirika;

ix) Serikali iongeze bajeti ya MKURABITA na kutoa kikamilifu na kwa wakati fedha inayotengwa, ili kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji wa ardhi na biashara za wananchi. Hadi mwezi Februari, 2018 MKURABITA ilikuwa imepokea asilimia 52.85 tu ya fedha yote iliyoidhinishwa katika mwaka huu wa fedha ambayo ilikuwa ni **shilingi bilioni 4.4**

x) Watendaji wa Halmashauri washirikiane na MKURABITA, katika kuandaa na kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi na hivyo kupunguza au kuepusha migogoro ya ardhi baina ya makundi ya watumiaji katika jamii;

xi) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) uwezeshwe kifedha ili kutanua wigo wa shughuli zake nchini na hivyo kuwafikia Wanawake na Vijana wengi zaidi;

xii) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, kiwezeshwe kukamilisha awamu ya mwisho ya ujenzi wa jengo ambao unaendeleo katika Kampasi ya Tabora. Aidha, Kampasi iapatiwe vitendea kazi na watumishi wa kudumu ili kupunguza gharama za uendeshaji na kulipa watumishi wa mkataba na washiriki;

xiii) Serikali iandae utaratibu wa kuingiza somo la maadili katika Mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari ili kujenga kizazi

chenye maadili na uzalendo ambacho kitachukia na kupinga vitendo vya rushwa;

xiv) Serikali itoe upendeleo wa mgawo wa watumishi watakaoajiriwa kwa baadhi ya Halmashauri ambazo maeneo ambayo yamebainika kuwa na upungufu mkubwa wa Watumishi, wa kati ya asilimia 32 hadi 65.

xv) Serikali iiwezeshe kikamilifu Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kukusanya na kuhifadhi taarifa na kumbukumbu muhimu kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Miongoni mwa njia za kukusanya taarifa hizo ni kutembelea na kuhoji watu wenye umri mkubwa ambao wameshuhudia mambo mengi ambayo ni muhimu kwa taifa na vizazi vijavyo;

xvi) Serikali iimarishe kampasi za Chuo cha Utumishi wa Umma zilizopo kabla ya kuanzisha nyingine, ili kuwezesha chuo hicho kutoa huduma bora; na

xvii) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) itoe mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kiutendaji na hivyo kuepusha migongano isiyo ya lazima ambayo inaweza kuibuka.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna mnavyoendesha shughuli za Bunge. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge wote kwa kuchaguliwa tena kuendelea na nafasi zao. Hii ni ishara kwamba, utendaji wao katika kipindi kilichopita ulikuwa mzuri na ndiyo umewapa imani Waheshimiwa Wabunge kuweza kuwachagua tena.

Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati kwa kutuchagua tena mimi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Mwanne Ismail Mchemba (Mb) ili tuendelee kuongoza Kamati kwa kipindi kilichosalia cha uhai wa Bunge. Hii ni ishara kwamba, wanatuamini na wako tayari kushirikiana nasi katika kutekeleza shughuli za Kamati. Tunawaahidi kwamba tutaenzi imani na ushirikiano wao kwetu, na njia pekee ya kufanya hivyo ni kuwatumikia kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii ina mafungu mengi ya Bajeti (mafungu 36) ambayo inayashughulikia, na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi wakati mwingine hadi jioni.

Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, kwani walitekeleza wajibu wao kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hii ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla.

Kwa umuhimu wa namna ya pekee ningetamani sana kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba,Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
6. Mhe. Hamad Salim Maalim,Mb
7. Mhe. Waitara Mwita Mwikwabe,Mb
8. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate,Mb
9. Mhe. Mwatum Dau Haji,Mb
10. Mhe.Saada Mkuya Salum,Mb
11. Mhe. Salum Khamis Salum,Mb
12. Mhe. Venance Methusela Mwamoto,Mb
13. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb
14. Mhe. Anna Joram Mhagama, Mb
15. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb

16. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
17. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
19. Mhe. Joseph Raman Selasini, Mb
20. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
22. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
23. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
24. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
25. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Utumishi, Dr. Lauren Ndumbaro kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Catherine Kitutu, kwa kuratibu vizuri

shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. Vilevile, nawashukuru watumishi wote wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, wakiongozwa na Bi. Hanifa Masaninga, kwa kuandaa na kutoa vitabu vya taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S.Rweikiza (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA**

11 Aprili, 2018